

ZANZIBAR LEO JUMATA TU 12, FEBRUARI 2024 UK-6

PAC yaipongeza e-GA kufanikisha malengo ya serikali

NA SAIDA ISSA, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC), imeipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuendeleza tafiti na bunifu zinazochagiza usanifu na utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA inayoleta tija kwa taifa.

Pongezi hizo zimetolewa na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya PAC, Japhet Hasunga, mara baada ya kamati hiyo kufanya ziara fupi ya kutembelea Kituo Cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC) cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kilichopo jijini Dodoma.

Hasunga alisema e-GA imewezesha serikali kuokoa fedha nyingi kwa kusanifu na kutengeza mifumo ya TEHAMA inayotumika katika taasisi mbalimbali za umma ambapo, hapo awali mifumo hiyo ilinunuliwa kutoka nje ya Tanzania kwa gharama kubwa.

Kadhhalika alibainisha kwamba, uzoefu unaonesha kuwa katika taasisi mbali mbali za umma walizozitembelea siku za nyuma kulikuwa na changamoto nyingi kuhusu suala la mifumo ya TEHAMA.

"Moja ya jambo lililokuwa linatusumbua sana kamati hii ni taasisi nyingi kununua mifumo ya TEHAMA kutoka nje, lakini misimbo (source code) inabaki kwa waliotengeneza mifumo na wakati mwingine mifumo hiyo baada ya muda haitumiki tena hivyo sisi tumekuwa tukisema hakuna thamani ya fedha katika ununujaji wa mifumo hiyo ambayo tumetumia gharama kubwa kuinunua", alifafanua Hasunga.

Hasunga alisema kuwa licha ya mifumo hiyo kununuliwa kwa gharama kubwa lakini haikuwa na matokeo yaliyotarajiwa hivyo kuzingiza taasisi hizo katika matumizi mabaya ya fedha.

"Kuna taasisi zilizinunua mifumo kwa zaidi ya bilioni 30, lakini mfumo haujamaliza mwaka wanautupa, na tulipowauliza walisema waliona mfumo huo haufai hivyo wameamua kutafuta mfumo mwingine", alisema Hasunga.

Aliongeza kuwa katika ziara hiyo kamati imebaini kwamba, e-GA imesaidia kusanifu na kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA nchini, ambayo imezisaidia taasisi za umma kuokoa

fedha nyingi zilizokuwa zinatumiwa kununua mifumo kutoka nje ya nchi.

Katika kuhakikisha mifumo ya TEHAMA Serikalini inawasiliana na kubadilishana taarifa, Hasunga ameitaka e-GA kuhakikisha kwamba taasisi nyingi zaidi zinaunganishwa katika Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB), ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za serikali mtandao kwa wananchi.

"Tumefurahi sana kuona namna mifumo mbalimbali inavyowasiliana, tujitahidi tufike angalau asilimia 80 tu tutakuwa tumefika pazuri kwa sababu tutapunguza gharama na malalamika katika utaji wa huduma za serikali mtandao", alisema Hasunga.

Naye Mjumbe wa kamati hiyo, Ester Matiko, aliipongeza e-GA na kushauri serikali kuwekeza zaidi kwa vijana ili kuwezesha nchi kuingia katika teknolojia za kisasa ikiwemo 'blockchain' na akili bandia.

"Uwepo wangu hapa nimepata vitu vingi vya ziada ambavyo nilikuwa sivijui, hivyo niombe serikali na taasisi zake wawaangalie vijana hawa na wengine ambao wapo huko nje kuhakikisha tunawasaidia na wanatumika ipasavyo katika ujenzi wa Serikali Mtandao", alisema Matiko.

Kwa upande wake Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, aliomba kamati hiyo kuwa Mabalizi wa kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika kuhakikisha inakuza jitahada za serikali mtandao nchini.

Aidha Kikwete alieleza kamati hiyo kwamba kituo hicho cha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa serikali mtandao kina eneo finyu, hivyo e-GA inahitaji kutengewa bajeti ili kujenga miundombinu (majengo) yake katika eneo la Kikombo.

"Kituo chetu kinatakiwa kipate nafasi kubwa sana, mmejionea wenyewe maabara zetu ni ndogo sana hivyo serikali (Wizara) itakapoleta bajeti huko bungeni tunaomba mazingatie jambo hili", alisema Kikwete.

Nae Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba, alishukuru kamati hiyo kwa kutembelea kituo hicho na kuaahidi kutekeleza maelekezo, maoni na ushauri uliotolewa na wajumbe wa kamati hiyo ili kuimarisha bunifu na tafiti za serikali mtandao.